# ADM-A012-MATUKIO YA UPENDELEO NA NEMBO ZA CHUKI (WANAFUNZI WOTE WANAKUBALIKA)

## SERA YA UONGOZI

### UTENDAJI KWENYE UONGOZI

### UFUPISHO

Wilaya ya Shule za Salem Keizer inaamini kwamba wanafunzi wote wana haki ya elimu yenye viwango vya juu bila ubaguzi au unyanyasi kulingana na rangi, dini, jinsia, utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kijinsia, ulemevu au asili ya utaifa. Maeneo ya wilaya yatakuwa ni sehemu salama naya ukaribisho ambapo wanafuzi wote, wafanyakazi, na wageni wanahaki ya kujifunza, kufanyakazi na kushiriki katika mazingira salama na huru kutoka kwenye ubaguzi, unyanyasaji na vitisho kulingana na rangi, dini, jinsia, utambulisho wa kijinsia, ulemavu au asili ya utaifa.

### MAANA

**Uhuishaji**
Hisia ya chuki au hasiria kwa mtu au kitu.

**Matukio ya Upendeleo**
Usemi wa chuki kwa mtu mwingine, kuhusiana na rangi ya mtu mwingine, rangi, dini, utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu au asili ya kitaifa ambayo uchunguzi wa jinai au mashtaka haiwezekani au hayafai. Matukio ya upendeleo yanaweza kujumuisha lugha ya dharau au tabia inayoelekezwa au kuhusu vikundi vyovyote vya idadi ya watu.

**Mtu Aliyeathiriwa**
Mtu ambaye anadaiwa kuwa mwathirika wa tabia ambayo inaweza kuwa tukio la upendeleo. Hii ni pamoja na mtu ambaye tukio lilielekezwa pamoja na wanafunzi au wafanyakazi katika jamii kubwa ya shule ambayo inaweza kuathiriwa na tukio hili.

**Nembo za Chuki**
Nembo, picha au kitu ambacho kinaonyesha uhuishaji kwa misingi ya rangi, dini, utambulisho wa kijinsia, mwelekeo wa kijinsia, ulemavu au asili ya kitaifa ikiwa ni pamoja na kitanzi, alama za nembo ya itikadi ya neo-Nazi na bendera ya vita ya Confederacy, na ambayo onyesho lake lina uwezekano mkubwa wa kusababisha usumbufu mkubwa wa kuingiliana na shughuli za shule, au kuna uwezekano mkubwa wa kuingilia haki za wanafunzi wa kuwanyima ufikiaji kamili wa huduma, pamoja na fursa zinatolewa na shule.

**Mali za Shule**
Mali zote zilipo kwenye udhibiti wa wilaya

**Programu ya Elimu**
Programu yoyote, huduma, shule au shughuli zilizofadhiliwa na wilaya

### MAELEKEZO

1. Wilaya ya shule inakataza matumizi au kuonyesha alama zozote za chuki kwenye mali ya shule au katika mpango wa elimu isipokuwa pale inapotumika katika mtaala wa kufundishia ambao unaendana na viwango vinavyotakiwa kwenye elimu ya umma.

2. Katika kukabiliana na matumizi ya nembo ya chuki au matukio ya upendeleo, wilaya itachukua hatua zisizo za kinidhamu wakati wowote inapotakikana.

3. Wilaya inakataza kulipiza kisasi dhidi ya mtu binafsi kwa sababu mtu huyo ana taarifa nzuri ambazo huyo anaamini ni ushahidi wa ukiukaji wa sheria ya serikali, kanuni au shirikisho.

4. Hakuna chochote katika sera hii kinachokusudiwa kuingilia matumizi halali ya vifaa vya wilaya kulingana na kukodisha au leseni.

5. Wilaya itatumia utaratibu wa ADM-P010 Kuripoti Matukio ya Upendeleo na Nembo ya Chuki – Ili kuchanganua ripoti au malalamiko ya upendeleo.

**KUTEKELEZWA**

- Sera hii inatumika kwa wafanyakazi wote, walimu mbadala, wanaojitolea, wakandarasi, na mawakala wa Wilaya.

**NYARAKA WASHIRIKA**

- ADM-P010 - Taarifa ya Matukio ya Upendeleo na Nembo ya Chuki
- ADM-P010 - Taarifa ya Matukio ya Upendeleo na Nembo ya Chuki (Kihispania)

**MAMLAKA YA KIBALI**

- Utendaji kwenye Uongozi

**HISTORIA YA MARUDIO**

- 11/23/2020 - Sera ilitengenezwa
- 04/12/2021 - Imesasishwa kwa mifano ya alama za chuki na taarifa
- 07/17/2024 - Imesasishwa kufikia kielezo kinachopatikana na mpangalio na sera ya mfano ya OSBA